OFISI YA RAISI,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI
SHULE YA SEKONDARI MENGELE
OFISI YA MKUU WA SHULE
S.L.P 145, CHIMALA
SIMU: 255759817548

Tarehe 10 **APRIL** 2022

KUMB.NA.MSS/JI/K.5/22/1/01.
JINA LA MWANAFUNZI
……
ANUANI ……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO MWAKA 2022

1. Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano, shule ya sekondari Mengele Mwaka **2022** tahasusi ya **PCM/CBG.**

2. **MAHALI SHULE ILIPO**
   Shule ya sekondari **MENGELE** iko mji wa **CHIMALA**, wilaya ya **MBARALI** mkoa wa **MBEYA**.Kama unatokea Mbeya mjini, panda magari yanayokwenda Rujewa (Pandia Nane nane au Uyole) utashukia **chimala-stendi mpya** na chukua usafiri wa bodaboda hadi shuleni. Wanaotokea Songea,Njombe,Dodoma,Dar-es-salaam nk. kuja Mbeya shuka **chimala –stendi mpya** kisha chukua usafiri wa bodaboda hadi shuleni. Nauli toka mbeya mjini mpaka chimala ni tsh 3000=. Usafiri unaopatikana kwa urahisi muda wote kuja shuleni ni Pikipiki kwa bei ya tsh 1000=.

3. Hali ya hewa ya Mengeleni ya joto (bonde la ufa Usangu) wakati wa mchana na baridi wakati wa usiku.

4. Unatakiwa kufika shuleni **tarehe** iliyotangazwa na OR-TAMISEMI asubuhi au kabla. Masomo yataanza tarehe shule itakapo funguliwa asubuhi. Tafadhali fika shuleni ukiwa na vifaa na michango yote uliyoagizwa.
5. Uaminifu, utii, juhudi, maarifa na nidhamu safi kwa ujumla vitakuwezesha kufanikiwa katika taaluma na kujijengea tabia nzuri na mwenenendo mzuri.

MENGELE SEC SCHOOL 2022

1.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1.1. SARE YA SHULE

i) Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
ii) Sketi mbili rangi ya **DAMU YA MZEE** ndefu za linda box mbele na nyuma kitambaa kigumu (Zifike kifundo cha unyayo). Kipande cha kitambaa imeambatishwa.
iii) Tai Damu ya mzee iwe ya wastani (Isiwe ndefu sana wala fupi sana)
iv) Viatu vya ngozi rangi nyeusi(vya kamba na visiwe vya mchongoko na vyenye visigino vifupi)
v) Soksi jozi mbili nyeupe
vi) Godoro ft 2 ½ x 6
vii) Sweta la shingo ya "V" rangi kijani kibichi
viii) Kwa wasichana wa Kiislam. Hijabu nyeupe na nusu kanzu tetroni isiyoangaza pamoja na sketi ndefu inayofika kwenye kongo mbili za miguu.
ix) Shamba dress (gauni) Mshono solo kuanzia mbili rangi ya dark bluu ifike kwenye kifundo cha unyayo.
x) Kila mwanafunzi aje na mavazi ya michezo yaani nguo zitakazo msitiri wakati wa michezo tracksuit rangi lightblue na t-shirt (Taifa Stars rangi ya light bluu), raba, n.k
xi) Tshirt ya shule (zinapatikana shuleni kwa gharama y ash 15,000)

1.2. MAHITAJI YA WOTE

i) Mashuka mawili rangi ya pink na bluu bahari
ii) Foronya mbili(2) za mito rangi ya pinki na bluu bahari
iii) Chandarua cha mbu
iv) Blanketi moja jepesi
v) Sanduku la chuma na kufuri lake
vi) Ream za karatasi 2 zikabidhiwe shuleni wakati wa kuripoti.
vii) Dissecting kit kwa wanafunzi waliochaguliwa kwa tahasusi /combination ya CBG
viii) Laboratory coat (Koti la maabara) rangi nyeupe linalozidi magotini
ix) Scientific calculators (CASIO Fx 991) kwa wanafunzi wote
x) Vyombo vya chakula(sahani, bakuli,kijiko, na kikombe) Ndoo ndogo moja
xi) Daftari kubwa (counter books) zaidi ya 10
xii) Mkebe,biki,rula nk.
xiii) Kwanja 1, jembe 1, fagio ya ndani (brush ngumu) 1, fagio ya ndani (brush laini) 1 , chelewa 1, reki 1 na Panga 1

MENGELE SECSCHOOL 2022

xiv) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika aliyopangiwa mwanafunzi
xv) NAKALA YA HATI YA MATOKEO (**RESULT SLIP**) YA KIDATO CHA NNE
xvi) Fomu ya afya (Medical examination form)iliyojazwa na kuthibitishwa na daktari wa Hospitali ya Serikali.(imeambatanishwa mwishoni)

1.3. ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) Ada ya Shule kwa mwaka ni Tshs 70.000/= na unaweza kulipa kiasi cha Tshs 35,000/= kwa nusu muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.
b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni;

i) Shilingi **15,000**/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii) Shilingi **6,000/=** kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii) Shilingi **20,000/=** kwa ajili ya taaluma
iv) Shilingi **30,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi, na vibarua wengine
v) Shilingi **2,000/=** kwa ajili ya nembo ya shule
vi) SHILINGI **20,000** kwa ajili ya mitihani ya kujipima (MOCK)
vii) Shilingi **5,000/=** fedha ya Tahadhari (**haitarejeshwa**)
viii) Shilingi **10,000/=** kwaajili ya huduma ya kwanza.

Fedha za ADA na michango zilipwe kwenye akaunti ya Shule
Na 61101100020 NMB jina la Akaunti ni **MENGELE SECONDARY SCHOOL** kisha uje na risiti (PAY IN SLIP) original yenye jina la mwanafunzi.

c) Shilingi **50,400** kwa ajili ya bima ya afya ya NHIF iwasilishwe ofisi ya uhasibu siku ya kuripoti shuleni. (Mwanafunzi mwenyewe bima ya afya (NHIF) aje nayo, yeye hatachangia).

MENGELE SECONDARY SCHOOL 2022

2.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

2.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa **walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na viranja wa shule, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla** ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi kufika shuleni na katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha mkuu wa shule ni kosa.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule. **Mwanafunzi anatakiwa kuoga kila siku, kukata nywele na kuzichana, kukata kucha, kupiga mswaki kila siku, na kuvaa vizuri wakati wote. Mitindo ya rasta, kalkiti, panki, kusuka, kutinda nyusi au kunyoa vipara hairuhusiwi kabisa. Aidha ni marufuku kuvaa mapambo kama vile mikufu, hereni, bangili, shanga, kofia, kupaka rangi kucha, wanja, rangi za midomo, kuvaa pete nk.**
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Kutunza mali za umma.
j) Kusimama na kusalimu walimu, wafanyakazi wote na wakubwa wanapopita ama kuongea nao.

2.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.
e) Makosa ya jinai
f) Kupiga au kupigana
g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

MENGELE SCHOOL 2022

h) Kudharau bendera ya Taifa
i) kuolewa
j) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
k) Kutoa mimba
l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
m) Kukataa adhabu kwa makusudi
n) Kuwa na simu ya mkononi
o) Kutembea, kushiriki na kwenda sehemu zifuatazo; **vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za kufikia wageni.**
p) Kutukana au kutumia lugha chafu.

3.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

a) Medical examination form (Ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali).
b) Fomu ya maelezo ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki migomo na kadharika
c) Tamko la mzazi

ZINGATIA

a) Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.
b) Mara tu mwanafunzi anaripoti shuleni aingie ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya kusajiliwa/kudahiliwa (Admission).

NAKUTAKIA MASOMO MEMA
KARIBU SANA MENGELE SEKONDARI UFUTE UJINGA
.....
PASKALIA . E. MAGANGA
MKUU WA SHULE

MENGELE SEC SCHOOL 2022

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF EDUCATION , SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATIONAL TRAINING
FORM 1
MEDICAL EXAMINATION FORM

MENGELE SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 145,
CHIMALA-MBEYA.
DATE ...../...../2022

REF: NO.MSS/MEF/Vol.02
MEDICAL OFFICER,
.....
.....

PART I

REF: FORM FIVE

ENTRANT.....
AGE ..... YEARS ..... SEX .....
Please examine the above named form one entrant as to his/her physical and mental fitness to persue secondary education at this school. The examination should include the following categories:-

1. Hemoglobin .....
2. P.V Bleeding .....
3. Sight .....
4. Blood pressure .....
5. Urine analysis .....
6. Stool examination .....
7. Pregnancy test .....
8. Skin diseases .....
9. Leprosy .....
10. Any deformity .....
11. Epilepsy .....
12. Pulmonary tuberculosis .....
13. Neurosis .....
14. Venereal diseases .....
15. Eye test .....
16. Ears .....
17. Chest .....
18. Spleen .....
19. Abdomen .....

MENGELE SEC SCHOOL 2022

20. Other diseases eg: physical defects or impairments infectious/chronic/family diseases
    ……

PART II

1. I have examine the above named form one Entrant and I certify that he/she is physical and mental fit/unfit to purse secondary education studies.
2. Other comments
    ……

Signature ……
Designation ……
Station ……
Date ……
Official stamp ……

NB: No student will be enrolled without certification of his/her physical and mental fitness.

MENGELE SEC SCHOOL 2022

FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

SEHEMU A (Ijazwe na Mwanafunzi)

JINA KAMILI(Kama kwenye result slip) .....
Tarehe ya kuzaliwa.....Kabila.....Dini/Dhehebu.....
tahasusi uliyochaguliwa.....Shule nitokayo.....
Mahali niishipo.....Mkoa.....Wilaya.....
Anwani yako: S.L.P.....

SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI

Jina la Baba/Mlezi.....kazi yake.....
Jinala Mama/Mlezi.....kazi yake.....
Wazazi/walezi wanaishi (wapi).....pamoja/wametengana.....
Anwani ya mzazi/mlezi: S.L.P.....
SIMU 1.....
SIMU 2.....

Wakati wa likizo zote nitakuwa kwa(mtaje).....Wapi.....
SIMU.....

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi:

Sahihi ya Mwanafunzi.....Tarehe.....

KUKUBALI NAFASI (Ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)

Mimi.....Nimesoma maagizo na taratibu za Shule na Wizara kwa makini, na kuzielewa na nipo tayari kuzifuata,Hivyo nakubali nafasi niliyopewa na nitafika Shuleni siku/tarehe husika kama zilivyopangwa

Sahihi:.....Tarehe.....

MENGELE SEC SCHOOL 2022

KUTOSHIRIKI MGOMO /FUJO /MAKOSA YA JINAI

(Ijazwe na mwanafunzimwenyewe)

MIMI……UMRI…….. NAAHIDI Kwamba nitakuwa mwadilifu na mwaminifu, na kwamba sita shiriki wala kusababisha/kuchochea mgomo kwa namna yeyote ile, na nitatoa taarifa kwa utawala pale nitakapoona viashiria vya mgomo/fujo au uvunjifu wa amani Shuleni .

Aidha naahidi kwamba hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na
kusimamishwa au kufukuzwa shule iwapo nitabainika kuwa nimeshiriki katika makosa
yaliyoainishwa katika kifungu hiki

JINA LA MWANAFUNZI……SAHIHI……TAREHE……
JINA LA MZAZI /MLEZI……SAHIHI……TAREHE…….

MENGELE SEC SCHOOL 2022

SEHEMU C

FOMU YA MZAZI KUKIRI /KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZA KUMLIPIAMWANAE ADA NA MICHANGO MINGINE

(IJAZWE NA MZAZI/MLEZI

MIMI.....ambaye ni.....wa mwanafunzi huyu(uhusiano)

Nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na Sheria za Shule katika fomu ya kujiunga na nipo tayari ajiunge na Shule hii, Nina ahidi kumtolea ada,michango na mahitaji mengine ili aweze kupata Elimu yake vizuri katika Shule hii. Aidha nitasaidiana na walezi/walimu wa Shule katika kumlea kijana huyu katika maadili mema, na kuitika wito wa kufika Shuleni pale nitakapohitajika.

Aidha taarifa zote za maendeleo ya taaluma za kijana huyu itanifikia zikitumwa kwa ;

Jina(mzazi/mlezi).....S.L.P.....

Anwani yangu ya kudumu ni ..... SIMU.....

Sahihi.....Tarehe.....

Ndugu zangu wanaoweza kumtembelea mwanafunzi picha, na namba zao za simu zimeorodheshwa hapa chini:

1. .....simu.....
2. .....simu.....
3. .....simu.....
4. .....simu.....

PICHA 1	PICHA 2	PICHA 3	PICHA 4

MENGELI SEC SCHOOL 2022

UWAPO SHULENI MWANAFUNZI UNATAKIWA KUZINGATIA YAFUATAYO;

1. Kila mwanafunzi anatakiwa ahudhurie maandalio ya jioni siku zote za wiki (jumatatu hadi Jumapili saa 1:30 hadi saa 4:00 Usiku.)
2. Ili kufanikisha maandalio ya jioni, kila mwalimu wa somo atakuwa anatoa kazi na kuhakikisha kuwa kazi hizo zimefanywa.
3. Walimu wa zamu watakuwa wanasimamia maandalio ya joini kikamilifu.
4. Kuthamini muda
5. Kuwahi katika shughuli za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku
6. Kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa
7. Siku ya kufungua shule, atokapo likizo mwanao anatakiwa kuripoti tarehe na muda aliopangiwa, iwapo atachelewa kufika tarehe na saa aliyopangiwa hatapokelewa. Mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni atalazimika kuja na mwanae shuleni ili apokelewe.
8. Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare ya shule wakati wote awapo ndani na nje ya mazingira ya shule.

A] Kila mwanafunzi azingatie mipaka ya shule Kama ifuatavyo:-
B] Kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kibali cha Mkuu wa shule
C] Kutotembelea sehemu zifuatazo isipokuwa Kwa kibali maalum Chumba cha walimu (staffroom), Ofisi za shule, Maabara, Jikoni,nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

.....
MKUU WA SHULE
0759817548

MENGELE SEC SCHOOL 2022

BAADHI YA VITABU MUHIMU KWA MWANAFUNZI KIDATO CHA TANO NA SITA

NO.	BIOLOGY	CHEMISTRY	PHYSICS	B/MATHEMATICS	GENERAL STUDIES	BASIC APPLIED MATHS
1.	Biological science	Ramsden Chemistry	Contemporary Physics	Tranta Math's	General Study for Advance (V)	Basic Applied Maths Form 5
2.	Understanding biology	Understanding Chemistry	Understanding Physics	S.chandi's Mathematics XI & XII	General Study for Advance (VI)	Basic Applied Maths Form 6
3.	S.chandi's BIOLOGY XI	S.chandi's CHEMISTRY XI	Roger's Physics	Pure Mathematics Volume 1 & 2	Contemporary Approach, G.S Notes 5&6	Basic Applied Maths Review
4.	S.Chandi's BIOLOGY XII	S.chandi's CHEMISTRY XII	S.chandi's PHYSICS XI & XII	Understanding Mathematics		
5.	Advanced Level Biology	Advanced Chemistry	Nelkon Physics	Mathematics Review Paper 1&2		
6.	Biology Review Paper 1&2	Chemistry Review Paper 1&2	Physics Review Paper 1&2			

Ni muhimu kwa mzazi kumnunulia mwanao baadhi ya vitabu tajwa hapo juu kwa kadiri utakavyoweza

NB; FOMU YA KUJIUNGA INAPATIKANA SHULENI
NAMBA ZA SIMU,
MKUU WA SHULE 0759817548,
MAKAMU MKUU WA SHULE 0762060756,

MENGELE SEC SCHOOL 2021